



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

Dar es Salaam, 18 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha uchambuzi na kuamua rufaa za Wagombea wa Ubunge na Udiwani. Hadi kufikia jana tarehe 17 Septemba, 2020, baada ya kupitia kumbukumbu zote za rufaa zilizowasilishwa, Tume inapenda kuufahamisha umma wa watanzania wote mambo yafuatayo-

Jumla ya rufaa zilizopokelewa - 616

|                        |   |     |
|------------------------|---|-----|
| a) Ubunge rufaa        | - | 160 |
| b) Udiwani rufaa       | - | 456 |
| c) Malalamiko          | - | 25  |
| d) Rufaa zilizojirudia | - | 44  |

Katika rufaa 160 za Ubunge zilizoamuliwa na Tume matokeo yake ni kama ifuatavyo -

|   |   |    |
|---|---|----|
| i) Wagombea waliorejeshwa ni                            | - | 66 |
| ii) Wagombea hawakurejeshwa ni                          | - | 32 |
| iii) Rufaa zilizokataliwa za kuomba kuenguliwa wagombea | - | 57 |
| iv) Rufaa zilizojirudia                                 | - | 5  |


**JUMLA** 160

Kuhusu taarifa ya awali ya wagombea walioteuliwa kama wagombea pekee walikuwa 18. Baada ya Tume kupitia rufaa zilizowasilishwa kutoka katika majimbo hayo, imerejesha wagombea 3 waliokuwa wameenguliwa katika majimbo ya Namtumbo, Bukene na Kavuu. Hivyo basi, majimbo hayo yataendelea na kampeni na uchaguzi utafanyika tarehe 28 Oktoba 2020.

Baada ya kupitia na kuamua rufaa mbalimbali, Tume imekubali rufaa tatu (3) za kuwaengua wagombea katika majimbo matatu. Kwa matokeo hayo wabunge waliopita bila kupingwa ni 18. Pia, Tume imepokea taarifa ya kujitoa kwa wagombea wa Ubunge kwenye Majimbo ya Chalinze na Madaba, hivyo kubakia wagombea pekee ambao wanakuwa wamepita bila kupingwa.

Kufuatia kumalizika kwa kipindi cha pingamizi na rufaa, wagombea waliopita bila kupingwa kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ni 20. Tume itawatangaza katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria.

Imetolewa na,

  
Dkt. Wilson M. Charles  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**